Kitabu Kikuu Cha Mungu (God's Great Book)

Na

Ellis P. Forsman

Kitabu Kikuu Cha Mungu

Na

Ellis P. Forsman

Octoba 19, 2011

Kitabu Kikuu Cha Mungu

Zaburi 19:1-14

Tunapoutafakari uzuri na mpangilio wa uumbaji…

Tunaauona utukufu wa Mungu kupitia kazi zake za mikono. Zaburi 19:1, "*Mbingu zauhubiri utukufu wa Mungu na anga laitangaza kazi ya mikono yake.*"

Tunaona ushahidi wa nguvu na Uungu wake. Rum. 1:20, "*Kwa sababu mambo yake yasiyoonekana tangu kuumbwa ulimwengu yanaonekana, na kufahamika kwa kazi zake yaani uweza wake wa milele na Uungu wake; hata wasiwe na udhuru.*"

Labda tunashawishiwa kukubaliana na wimbo, "Jinsi Ulivyo Mkuu!"

Wakati uumbaji unafunua mengi kumhusu Mungu, haituambii chochote kuhusu…

- Karama kuu ya Mungu na huruma.
- Watu wema wa Mungu jinsi anavyotaka tuwe.

Kujifunza mambo kama hayo, lazima tuangalie sehemu nyingine. Mungu amechagua kufunua hili kupitia kitabu chake, Biblia.

Je kitabu hiki kinalingana na kazi? Unaweza kumtarajia Mungu mkuu kutupatia kitabu kikuu; siyo?

Hakika, ameweza! Kwa Roho wake? Alivuvia kitabu kitabu kilicho na uwezo wa kuhitimisha mambo makuu!

Kwa mfano, ebu tuanze na sehemu moja ya Biblia…

Agano la Kale ni kuu kiasi gani!

Katika siku za Daudi.

Muongozo wa furaha ya kweli.

Zaburi 1:1-3, "*Heri mtu yule asiyekwenda katika shauri la wasio haaki; wala hakusimama katika njia ya wakosaji; wala haakuketi barazani pa wenye mizaha. Bali sheria ya BWANA ndiyo impendezayo, na sheria yake huitafakari mchana na usiku. Naye atakuwa kama mti uliopandwa kandokando ya vijito vya maji uzaao matunda yake kwa majira yake, wala jani lake halinyauki, na kila atendalo litafanikiwa.*"

Fadhila za neno la Mungu husiwa:

Huongoa nafsi.

Zaburi 19:7, "*Sheria ya BWANA ni kamilifu huburudisha nafsi. Ushuhuda wa BWANA ni amani, humtia mjinga hekima.*"

Humtia mjinga hekima.

Zaburi 19:7, "*…ushuhuda wa BWANA ni amani, humtia mjinga hekima.*"

Huufurahisha moyo.

Zaburi 19:8, "*Maagizo ya BWANA ni adili, huufurahisha moyo…*"

Huyatimia macho nuru.

Zaaburi 19:8, "*Maagizo ya BWANA ni adili, huufurahisha moyo, amri ya BWANA ni safi, huyatia macho nuru.*"

Kinadumu milele.

Zaburi 19:9, "*…hukumu za BWANA ni kweli, zina haki kabisa.*"

Ni haki na hakika pamoja.

Zaburi 19:9, "*…hukumu za BWANA ni kweli zina haki kabisa.*"

Ni za kutamanika kuliko dhahabu, nazzo ni tamu kuliko asali.

Zaburi 19:10-11, "*Ni za kutamani kuliko dhahabu, kuliko wingi wa dhahabu safi. Nazo ni tamu kuliko asali, kuliko sega la asali. Tena mtumishi wako huonywa kwazo, katika kuzishika kuna thawabu nyingi.*"

Thamani ya neno la Mungu hutafakarika.

Humsaidi kijana kusafisha njia zake.

Zaburi 119:9, "*Jinsi gani kijana aisafishe njia yake? Kwa kutii akilifuata neno lako.*"

Hukinga moyo dhidi ya dhambi.

Zaburi 119:11, "*Moyoni mwangu nimeliweka neno lako, nisije nikakutenda dhambi.*"

Hutia hekima kuliko maadui.

Zaburi 119:97-98, "*Sheria yako naipenda mno ajabu ndiyo kutafakari kwangu mchana kutwa, maagizo yako hunitia hekima kuliko adui zangu, kwa maana ninayo siku zote.*"

Humpa mtu uelewa zaidi kuliko wakufunzi na watu wa zamani.

Zaburi 119:99-100, "*Ninazo akili kuliko wakufunzi wangu wote, maana shuhudaa zako ndizo nizifikirizo. Ninao ufahamu kuliko wazee, kwa kuwa nimeyashika mausia yako.*"

Ni taa na mwanga unaoongoza njia za mtu.

Zaburi 119:105, "*Neno lako ni taa ya miguu yangu, na mwanga wa njia yangu.*"

Huleta amani kuu kwa wale waipendao.

Zaburi 119:165, "*Wana amani nyingi waipendao sheria yako, wala hawana la kuwakwaza.*"

Hii ndio thamani ya sehemu ndogo ya neno la Mungu, ilikuwepo kipindi cha siku za Daudi (labda kwanzia kitabu cha Mwanzo hadi Ruth).

Katika siku za Paulo.

Chanzo cha uvumilivu na faraja, ikiweka tumaini kwa Mkristo.

Rum. 15:4, "*Kwa kuwa yote yaliyotangulia kuandikwa yaliandikwa ili kutufundisha sisi; ili kwa saburi na faraja ya maandiko tupate kuwa na tumaini.*"

Ikitumika kama mifano, yakaandikwa ili kutuonya.

1 Kor. 10:11, "*Basi mambo hayo yaliwapata wao kwa jinsi ya mifano, yakaandikwa ili kutuonya sisi tuliofikiliwa na miisho ya zamani.*"

Kama ilivyo maandiko yote yamevuviwa na Mungu, inafaa kwa njia nyingi.

2 Tim. 3:14-17, "*Basi wewe ukae katika mambo yale uliyofundishwa na kuhakikishwa, kwa maana unajua ni akina nani ambao ulijifunza kwao; nay a kuwa tangu utoto umeyajua maandiko matakatifu, ambayo yawezaa kukuhekimisha hata upate wokovu kwa imani iliyo katika Kristo Yesu. Kila andiko lenye pumzi ya Mungu lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishawa apate kutenda kila tendo jema.*"

- Humfanya mtu kuwa na akili ukizingatia wokovu kwa imani ndani ya Kristo.
- Hufaa kwa mafundisho, kuonya, kuadabisha katika haki.
- Humsaidia mtu wa Mungu kukamilika, katika kutenda kila tendo jema
- Mkristo anaweza asiwe chini ya Agano la Kale, lakini inabaki kuwa chanzo muhimu cha ukweli na furaha.

Kama hiyo ni kweli kulingana Agano la Kale, ni kiasi gani zaidi tunakuwa na ufunuo uliokamilika nay a mwisho wa neno la Mungu! Kwa maneno mengine…

Agano Jipya lina ukuu kiasi gani!

Ni neno lililohai.

Neno la Mungu ni hai na lina nguvu.

Heb. 4:12, "*Maana neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake.*"

Neno la Mungu hukata, hutambua.

Heb. 4:12, "*Maana neno la Mungu li…tena li jepesi kuayatambua mawazo na makusudi ya moyo.*"

Hii ni kwa sababu ni upanga wa Roho, kifaa anachotumia kuhukumu ulimwengu wa dhambi, haki, na hukumu.

- Yohana 16:7-8, "*Lakini mimi nawaambia iliyo kweli, yawafaa ninyi mimi niondoke, kwa maana mimi nisipoondoka, huyo Msaidizi hatakuja kwenu; bali mimi nikienda zangu nitampeleka kwenu. Naye akiisha kuja huyo atauhakikishia ulimwengu kwaa habari ya dhambi, na haki, na hukumu.*"
- Efe. 6:17, "*Tena ipokeeni chapeo ya wokovu, na upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu.*"

Ni neno linalotoa uzima.

Neno la Mungu linaweza kuokoa nafsi zetu.

Yak. 1:21, "*Kwa hiyo wekeeni mbali uchafu wote na ubaya uzidio, na kupokea kwa upole neno lile lililopandwa ndaani liwezalo kuziokoa roho zenu.*"

Neno la Mungu linaweza kufanya ukazaliwa mara ya pili na kukua kiroho.

1 Pet. 1:23-2:3, "*Kwa kuwa mmezaliwa mara ya pili; si kwa mbegu iharibikayo, bali kwa ile isiyoharibika; kwa neno la Mungu lenye uzima, lidumulo hata milele. Maana mwili wote ni kama majani, na fahari yake yote ni kama ua la majani. Majani hukauka na ua lake huanguka. Bali neno la Bwana hudumu hata milele. Na neno hilo ni neno lile jema lililohubiriwa kwenu. Ikiwa meonja ya kwamba Bwana ni mwenye fadhili.*"

Hii ni kwa sababu ya nguvu iliyomo katika injili ya Kristo.

Rum. 1:16-17, "*Kwa maana siionei haya injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza, na kwa Myahudi pia. Kwa maana haki ya Mungu inadhihirishwaa ndani yake toka imani hata imani; kama ilivyoandikwa mwenye haki ataishi kwa imani.*"

Ni neno linaloongoza maisha.

Ikizaa imani inayofaa katika kutembea kwetu kwenye maisha.

- 2 Kor. 5:7, "*(Maana twaenenda kwa imani si kwa kuona:)*"
- Rum. 10:17, "*Basi imani chanzo chake ni kusikia, na kusikia huja kwa neno la Kristo.*"

Ikiwajenga watakatifu katika kila kazi njema.

2 Tim. 3:16-17, "*Kila andiko lenye pumzi ya Mungu lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema.*"

Katika kumjibu shetani Yesu alinukuu:

Mat. 4:4, "*Naye akajibu akasema, imeandikwa mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu.*"

Hakupaswi kuwa na swali kwamba kitabu cha Mungu ni kikuu. Inatimiza hitaji letu kuu na kutupatia hitaji letu kuu. Lakini ebu tuzingatie…

Majibu yetu ni mazuri kiasi gani?

Je majibu yetu yanafaa?

Watu wengi (pamoja na Wakristo) "Kibiblia wamepotoka"!

Kama Israeli ya zamani, tunateseka kutokana na "njaa ya neno". Amosi 8:11-14, "*Angalia siku zinakuja asema Bwana MUNGU,*

ambazo zitaletaa njaa katika nchi; si njaa ya kukosa chakula wala kiu ya kukosa maji, bali ya kukosa kuyasikia maneno ya BWANA. Nao watatangatanga toka bahari hata bahari; na toka upande wa kaskazini hata upande wa mashariki; watapiga mbio wakienda huko na huko, kulitafuta neno la BWANA wasilione. Siku hiyo wana wali wazuri na wavulana watazimia kwa kiu. Na hao waapao kwa dhambi ya Samaria na kusema kama aishivyo Mungu wako, Ee Dani, na kama aishivyo njia ya Beer-sheba, hao nao wataanguka wasiinuke tena."

Njaa ya Israeli ililetwa na Mungu kwa utumwa wao. Familia zetu hutoa wenyewe kwa sisi wenyewe kuwakataa! Madhara bado yanafanana!

Vijana wetu huzimia kwa kiu! Wanaanguka na hawasimami ten! Maana wengi, hula "vyakula visivyo na huiano"!

Mfano:

- Wanasoma tu vifungu vilivyo chaguliwa, na mara nyingi hukataa Agano Jipya.
- Wakisoma tu ili kujithibitisha kwamba wako sahihi na wengine wanakosa. "Kitabu Kikuu Cha Mungu" kinafaa kwa majibu hayo yasiyofaa? Hapana! Jibu bora ni lipi?

Ni lazima tuipe thamani neno la Mungu.

Inathamani zaidi kuliko dhahabu na fedha. Zaaburi 119:72, "*Sheria ya kinywa chako ni njema kwangu, kuliko maelfu ya dhahabu na fedha.*"

Inathamani kama hazina kuu. Zaburi 119:162, "*Naifurahia ahadi yako kama apataye mateka mengi.*"

Je tunalichkulia neno la Mungu kuwa na thamani kuu kuliko pesa?

Lazima tusome neno la Mungu kwa bidii.

Tukiwa na nia ya kusubiri.

- Zaburi 119:131, "*Nalifunua kinywa change nikatweta, maana naliyatamani maagizo yako.*"

- 1 pet. 2:2, "*Kama watoto wachanga waliozaliwa sasa yatamanini maziwa ya akili yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu.*"

Tukiwa na dhamira ya kutii.

Yakobo 1:21-22, "*Kwa hiyo wekeni mbali uchafu wote na ubaya uzidio na kupokea kwa upole neno lile lililopandwa ndani liwezalo kuziokoa roho zenu. Lakini iweni watendaji wa neno wala si wasikiaji tu, hali mkijidanganya nafsi zenu.*"

Kwa maombi midomoni mwetu na mioyoni mwetu.

- Zaburi 119:18, "*Unifumbue macho yangu niyatazame maajabu yatokayo katika sheria yako.*"
- Zaburi 119:133, "*Uzielekeze hatua zangu kwa neno lako, uovu usije ukanimiliki.*"

Mikakati ya kweli ya kila siku ya usomaji wa Biblia katika roho kwafaa kwa majibu ya ukuu wa neno la Mungu!

Hitimisho

Ukitafakari uumbaji wa Mungu kunaleta jibu: Jinsi Ulivyo Mkuu!

- Mungu ni Uwepo wa Uwezo mkuu.
- Mungu ni Uwepo wa intelijensia mkuu.

Ukitafakari kitabu cha Mungu kikitoa jibu linalofanana: Jinsi Ulivyo Mkuu!

- Mungu ni Uwepo mkuu wa hekima na uelewa.
- Mungu ni Uwepo mkuu wa upendo na hurumaa.
- Mungu ni Uwepo mkuu wa haki.

Naomba kwamba somo letu lifanye angalau mambo mawili:

- Iongeze shukurani zako kwa ajili ya "Kitabu Kikuu cha Mungu".

- Hiuhishe hamu yako ili kuwa na bidii katika majibu yako kwalo.
    - Bidii nyingi katika kuisoma.
    - Bidii nyingi katika kuitii.

Mdo. 20:32, "*Basi sasa nawaweka katika mikono ya Mungu, na kwa neno la neema yake, ambalo laweza kuwajenda na kuwapa urithi pamoja nao wote waliotakaswa.*"

Ebu "Kitabu Kikuu cha Mungu" kikujenge, ili uweze kupokea hiyo ya ajabu: 1 Pet.1:4, "*…urithi usioharibika, usio na uchafu, usio nyauka, ulitunzwa mbinguni kwa ajili yenu.*"